**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**689** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2009**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama 30 kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Eleza maana ya neno "Zana za Kufundishia".

   (b) Orodhesha aina tatu (3) za zana za kufundishia zinazoweza kutumika katika somo hili.

2. (a) Taja sifa tatu (3) za andalo la somo bora.

   (b) Fafanua njia moja (1) ya kuongeza uwezo wa mtoto wa kufikiri kwa ubunifu.

3. (a) Bainisha hatua nne (4) za kuzingatia unapoandaa eneo la kuchezea.

   (b) Eleza kwa kifupi umuhimu wa malengo ya somo.

4. (a) Nini maana ya "Mbinu ya Kufundishia"?

   (b) Orodhesha misismsi minne (4) ya kuzingatia unapo mfanyia mtoto uchunguzi wa maendeleo.

5. (a) Fafanua faida nne (4) za kutumia zana za teknolojia (mfano, video) katika kufundisha somo hili.

6. Ainisha vitu vinne (4) vinavyoweza kutumiwa kama motisha katika kipindi cha Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

7. (a) Taja sababu tatu (3) za mwalimu kutumia njia ya kuuliza maswali darasani.

   (b) Bainisha kanuni mbili (2) za kuandaa ratiba ya mwaka ya shule.

8. (a) Eleza umuhimu wa kushirikisha wazazi katika mtaala wa elimu ya awali.

   (b) Taja aina mbili (2) za uchunguzi wa kitabibu zinazofaa kwa watoto wa shule.

9. (a) Orodhesha sifa nne (4) za mwalimu anayeweza kutumia njia ya ugunduzi kwa ufanisi.

10. (a) Eleza kwa kifupi faida mbili (2) za kufuata ratiba ya masomo.

    (b) Taja mambo mawili (2) yanayoashiria kuwa mtoto ana matatizo ya kusikia darasani.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. (a) Jadili mambo sita (6) ya kuzingatia unapotathmini ubora wa zana za kufundishia kabla ya kuzitumia darasani.

    (b) Fafanua faida nne (4) za kutumia vikundi vidogo wakati wa ufundishaji wa Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

12. (a) Eleza kwa kina umuhimu wa andalo la somo kwa mwalimu na kwa mwanafunzi. Toa faida tano (5).

    (b) Bainisha mambo matano (5) ya msingi ambayo mwalimu wa elimu ya awali anapaswa kuyajua kuhusu saikolojia ya mtoto.

13. (a) Kwa nini mwalimu anapaswa kuunganisha masomo katika kufundisha Vitendo vya Kujifunza Sayansi? Toa sababu tano (5).

    (b) Eleza maana na umuhimu wa kufanya utafiti wa kielimu kwa mwalimu wa darasa.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Jadili namna mwalimu atakavyotumia zana za kufundishia za asili kufundisha dhana ya "vitu vizito na vyepesi" kwa kutumia:

    (a) Mbinu ya Kujifunza kwa Vitendo.

    (b) Mbinu ya Maswali na Majibu.

15. (a) Fafanua maana ya "Ushirikishaji wa Jamii" katika elimu na jinsi unavyoweza kuboresha ufundishaji wa Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

    (b) Tofautisha Upimaji wa Utambuzi na Upimaji wa Utendaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

16. (a) Jadili hatua tano (5) za kufuata unapotaka kufanya Uchunguzi wa Maendeleo wa mtoto na kurekodi matokeo.

(b) Bainisha changamoto tano (5) zinazokabili upatikanaji wa rasilimali za kufundishia katika shule za msingi za Tanzania.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org